

23  
2028



# BARAZA LA TAIFA LA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA

MPANGO MKAKATI WA TAIFA WA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA (2023 - 2028)



# DIBAJI

---

Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa 2023 – 2028 ni Mpango wa tatu kutekelezwa chini ya Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Fedha. Mpango huu ni mwendelezo wa mafanikio yaliyofikiwa chini ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Pili ambao utekelezaji wake ulikamilika Desemba 2022.

Katika utekelezaji wa Mkakati wa pili wa Taifa wa Huduma Jumuishi za fedha, Tanzania imepata mafanikio makubwa yakiwemo ongezeko la asilimia ya watu wazima waliofikiwa na huduma rasmi za fedha kutoka asilimia 86 mwaka 2017 hadi 89 mwaka 2023, pamoja na ongezeko la watu wazima wanaotumia huduma rasmi za fedha kutoka asilimia 65 mwaka 2017 hadi asilimia 76 mwaka 2023. Kwa kiasi kikubwa, mafanikio haya yamechagizwa na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za fedha kwa njia ya kidijitali, uelewa wa huduma za fedha kwa watumiaji, na ushirikiano kati ya wadau wa huduma jumuishi za fedha wa sekta ya umma na binafsi.

Katika Mpango wa Tatu, dira yetu ni kuona rika la watu wazima na wafanyabiashara wote wanafikiwa na kutumia bidhaa na huduma mbalimbali za fedha zenye ubora wa hali ya juu ili kuboresha ustawi wa maisha yao ya kila siku. Ili kufanikisha utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea, Mkakati huu utatekelezwa kwa ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi, pamoja na wadau wa maendeleo.

Vilevile, Mpango huu umeweka mikakati mahsusi ya kuongeza idadi ya wananchi wanaotumia huduma za fedha kutoka katika makundi maalumu kama wanawake, vijana, wajasiriamali wadogo na wa kati, wakulima wadogo, wavuvi na watu wenye mahitaji maalumu ili kuongeza ushirikishwaji wa makundi hayo katika shughuli za kiuchumi na kuongeza mchango wake katika maendeleo ya uchumi wa Taifa.

Nina imani kwamba, mbali na kuweka vipaumbele katika makundi maalumu,

utekelezaji wa Mpango huu pia utasaidia watumiaji wa huduma za fedha nchini kufikiwa na watoa huduma ili kuwapa fursa ya kutumia aina mbalimbali za bidhaa na huduma fedha zilizo na ubora wa hali ya juu. Ili kufikia azimio hili, Serikali na sekta binafsi tutashirikiana kuweka mazingira wezeshi kwa watoa huduma za fedha na kuongeza matumizi ya teknolojia katika kufikisha huduma za fedha kwa wananchi.

Nimatarajio yangu kuwa, taasisi za umma na za binafsi zinazotekeleza Mpango huu, zitaendelea kushirikiana na wadau wa huduma jumuishi za fedha nchini ili kufikia malengo tuliyojiwekea kwa nia ya kuleta ustawi wa sekta ya fedha na kufikia uchumi jumuishi nchini.



**Bw. Emmanuel M. Tutuba**

Mwenyekiti, Baraza laTaifa la Huduma Jumuishi za Fedha

# UTANGULIZI

---

Mpango Mkakati wa Tatu wa Huduma Jumuishi Taifa wa Ujumuishaji za Fedha utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano kuanzia mwaka 2023 hadi 2028. Hii ni mwendelezo wa Mkakati wa Pili, uliotekelwa kuanzia mwaka 2018 hadi 2022 ambao ulijikita katika kuimarisha utumiaji wa bidhaa na huduma rasmi za fedha. Vilevile, Mkakati wa sasa utaendelea kutekelezwa kwa utaratibu wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuhakikisha rika la watu wazima na wafanyabiashara wote wanafikiwa na kutumia bidhaa na huduma mbalimbali rasmi za fedha zenye ubora wa hali ya juu kwa gharama nafuu.

## UMUHIMU WA MKAKATI WA TAIFA WA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA

---

Katika kuendelea kutatua changamoto za huduma jumuishi za fedha nchini, Tanzania imeandaa Mkakati huu ili kuwezesha wananchi wote kutumia bidhaa na huduma rasmi za fedha. Utekelezaji wa Mkakati huu ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Mpango wa Dira ya Muda Mrefu wa Tanzania 2011/12 - 2025/26, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, na Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha 2020/21 - 2029/30. Hivyo, ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi katika utekelezaji wa Mkakati huu unatarajiwa kuwa chachu ya maendeleo ya sekta ya fedha, ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa.

# TASWIRA YA SEKTA YA FEDHA

Sekta ya fedha ya Tanzania inajumuisha sekta ndogo ya benki, huduma ndogo za fedha, bima, masoko ya mitaji na hifadhi ya jamii kama inavyoonekana kwenye Kielelezo 1.

## Kielelezo 1: Takwimu za Mwonekano wa Sekta ya Fedha Disemba 2022



### Sekta ya Kibenki

Benki 44 | Matawi 981 | Mawakala 75,234  
Taasisi za karadha 5



### Sekta ya Huduma Ndogo za Fedha

#### Tanzania Bara

Taasisi za wakopeshaji wadogo 1,095 | SACCOS 759  
Vikundi vya kijamii vya fedha 34,127

#### Zanzibar

Taasisi za wakopeshaji wadogo 4 | SACCOS 219



### Sekta ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

- Kampuni zilizosajiliwa kwenye soko la hisa 28
- Kampuni zenye leseni ya biashara 16
- Washauri wa uwekezaji 19
- Wasimamizi wa fedha 11
- Mifuko ya uwekezaji wa pamoja 10
- Watunzaji wa mali 6
- Kampuni zenye leseni biashara ya dhamana 8
- Washauri wateule 6



### Sekta ya Bima

Kampuni 36 | Mawakala 1,019 | Madalali 110  
Wathamini 46 | Benki zinazotoa huduma ya bima 28




### Sekta ya Hifadhi ya Jamii

Mifuko ya pensheni kwa sekta rasmi 3 | Mifuko isiyo ya pensheni 2 | Mfuko wa sekta isiyorasmi 1 | Mifuko ya hiari 25

## HALI YA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA TANZANIA

Hadi kufikia 2023, upatikanaji na utumiaji wa bidhaa na huduma rasmi za fedha uliongezeka hadi kufikia asilimia 89 na 76 mtawalia, ukilinganisha na upatikanaji wa bidhaa na huduma za fedha kwa asilimia 86 na 65 mtawalia kwa mwaka 2017. Ongezeko la upatikanaji wa vituo vya utoaji wa huduma za fedha na watumiaji wa huduma rasmi za fedha umechangiwa na mambo mbalimbali ikiwemo; uwepo wa sera na sheria wezeshi katika sekta ya fedha, matumizi ya mifumo ya kidigitali katika utoaji wa huduma za fedha, kuongezeka kwa uelewa wa masuala ya elimu fedha kwa watumiaji wa huduma za fedha na ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi katika kutatua changamoto za sekta ya fedha.



Huduma za kibenki



Huduma zisizo za kibenki



Huduma zisizo rasmi



Wasiotumia huduma za fedha

# VIKWAZO NA FURSA ZILIZOPO KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA TATU

---

Kwa mujibu wa ripoti ya Tathmini ya Mkakati wa Pili wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha na matokeo ya utafiti wa Finscope kwa 2023, vifuatavyo ni vikwazo, fursa na viwezeshi katika kufikia malengo tuliyojiwekea:

## Vikwazo

- Uhaba wa vitambulisho vya Taifa na hasa kwa vijana;
- Miundombinu duni ya teknolojia ya mawasiliano;
- Umiliki mdogo wa simu janja;
- Changamoto za kisera na kisheria katika sekta ya fedha;
- Uwepo kwa bidhaa na huduma za fedha zisizoendana na mahitaji ya wateja;
- Matumizi madogo ya huduma za fedha za kwa njia ya kidijitali;
- Elimu duni ya masuala ya fedha kwa wananchi; na
- Gharama kubwa ya bidhaa na huduma za fedha.

## Fursa

- Matumizi ya teknolojia na ubunifu;
- Utekelezaji wa Sera ya huduma ndogo za fedha na Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha;
- Uwepo wa mradi wa huduma ya umeme vijijini;
- Uwepo wa mifumo ya kitaifa ya malipo na taarifa za wakopaji; na
- Uwepo wa miongozo na mifumo ya kulinda haki za watumiaji wa huduma za fedha.

## Viwezeshi

- Uwepo wa mifumo ya taarifa za watumiaji wa huduma za fedha;
- Uwepo wa kanzi data za taarifa za watu binafsi na makampuni itakayotumiwa na watoa huduma za fedha kuthibitisha taarifa za wateja wao;
- Uwepo wa mifumo ya kidijitali ya malipo ya Taifa;
- Upatikanaji wa bidhaa na huduma mbalimbali za fedha na za bei nafuu; na
- Uwepo wa program za utoaji wa elimu fedha.



# MPANGO WA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA 2023-2027

## Maana ya Huduma Jumuishi za Fedha

Huduma Jumuishi za Fedha ni upatikanaji na matumizi endelevu ya bidhaa na huduma mbalimbali rasmi za fedha zenye ubora wa hali ya juu na gharama nafuu kwa mtu binafsi au biashara ili kuboresha ustawi wa fedha na viwango vya maisha

## Dira

Watanzania watu wazima na biashara zao kuweza kufikiwa na kutumia bidhaa na huduma mbalimbali za fedha zenye ubora, gharama nafuu, zinazoboresha kipato na ustawi wa fedha.

## Misingi ya Utekelezaji

Utekelezaji wa Mpango Mkakati huu utazingatia misingi mitatu ambayo ni: wepesi wa kubadilika kutokana na mazingira, ushirikiano wa wadau wa sekta ya umma na binafsi pamoja na maamuzi yanayotokana na taarifa sahihi na tafiti.

## Malengo ya Kimkakati

Mkakati huu umeweka malengo manne ya kimkakati ambayo ni kuwezesha:

- Kupatikana kwa huduma za fedha na bidhaa kwa wote;
- Kuongeza matumizi ya aina mbalimbali za bidhaa na huduma za fedha;
- Kuimarisha/kuhakikisha/kuwezesha ubora wa bidhaa na huduma za fedha; na
- Kuimarisha ustawi wa fedha wa watu binafsi na biashara

## Viwezeshi Muhimu Katika Utekelezaji

Ili kupanua wigo wa huduma jumuishi za fedha nchini, Mkakati huu umeanisha viwezeshi vinne ambavyo ni muhimu katika kusaidia kupunguza pengo la watumiaji wa huduma rasmi za fedha na kuimarisha ustawi wa fedha wa Watanzania. Viwezeshi hivyo ni:

- Matumizi ya teknolojia na kuchochea ubunifu katika upatikanaji na matumizi ya bidhaa na huduma za fedha;
- Mazingira wezeshi ya sera, sheria, kanuni na miongozo;
- Utoaji wa elimu ya fedha na utatuzi wa malalamiko ya watumiaji wa bidhaa na huduma za fedha; na
- Kuongeza na kuboresha miundombinu ya taarifa na takwimu za watu binafsi na wafanyabishara.

## Maeneo ya Kipaumbele

Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kwanza na wa Pili wa huduma jumuishi za fedha nchini, baadhi ya makundi ya watu yameendelea kuachwa nyuma katika kupata fursa ya kufikiwa na watoa huduma au kutumia huduma za fedha nchini. Makundi haya ni pamoja na wanawake, vijana, watu wenye mahitaji maalumu, wakulima wadogo, wavuvi na wafanyabiashara wadogo na wa kati.

Kwa mantiki hii, Mpango Mkakati huu unatoa kipaumbele kwa makundi haya, ili kufanikisha utekelezaji wa malengo ya kimkakati. Maelezo ya uchambuzi wa hali ya huduma jumuishi za fedha, changamoto na fursa kwa kila kundi yamefafanuliwa katika kielelezo 2.

Kielelezo 2: Vipaumbele, Fursa na Changamoto za Makundi Maalumu

Makundi ya Kipaumbele	Fursa	Changamoto
Wanawake	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ongezeko la watu wanaotumia simu za mkononi.</li> <li>• Ongezeko la vikundi vya kijamii vya kutunza amana na kutoa mikopo kwa wanawake.</li> <li>• Uwepo wa Mfuko wa Wanawake</li> <li>• Uwepo wa mipango ya Serikali kuwezesha wanawake.</li> <li>• Uwepo wa Kamati ya Masuala ya Wanawake ya huduma jumuishi za fedha.</li> <li>• Kuongezeka kwa idadi ya wanawake Wajasiriamali.</li> <li>• Uwepo wa mpango wa Taifa wa usawa wa kijinsia na kamati ya Taifa ya Ushauri wa Masuala ya Kijinsia</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mila, desturi na tamaduni zisizofaa.</li> <li>• Wanawake kutokuwa na haki katika kumiliki mali.</li> <li>• Elimu ndogo ya fedha.</li> <li>• Pengo kubwa la kipato kati ya wanawake na wanaume.</li> <li>• Wanawake wengi kushiriki katika shughuli zisizo rasmi za kiuchumi.</li> <li>• Kiwango cha chini cha elimu na uwezo wa biashara.</li> <li>• Uelewa mdogo wa wa watoa huduma kuhusu mahitaji ya fedha ya wanawake na masuala ya kitabia.</li> <li>• Ushiriki mdogo wa wanawake katika majukumu ya uongozi katika taasisi za fedha.</li> </ul>

Makundi ya Kipaumbele	Fursa	Changamoto
Vijana	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Idadi ya vijana inachukua asilimia 59 ya watu wazima nchini.</li> <li>• Matumizi makubwa ya teknolojia ya fedha.</li> <li>• Kuwepo kwa programu za kuongeza kasi ya ubunifu kwa vijana.</li> <li>• Kuongezeka kwa idadi ya wajasiriamali vijana</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Viwango vya chini vya mapato kwa vijana ambavyo vinapunguza umiliki wao wa mali.</li> <li>• Ukosefu wa vitambulisho vya taifa kwa vijana chini ya miaka 18.</li> <li>• Ukosefu wa taarifa za mikopo.</li> <li>• Ujuzi duni wa usimamizi wa fedha.</li> <li>• Vijana wengi hushiriki katika shughuli zisizo rasmi za kiuchumi.</li> </ul>

Makundi ya Kipaumbele	Fursa	Changamoto
Biashara Ndogo na za Kati	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Uwepo wa mikakati ya Serikali kwa ajili ya maendeleo ya Biashara Ndogo na za Kati.</li> <li>• Kuwepo kwa teknolojia ya fedha ya kidijitali.</li> <li>• Kuwepo kwa dhamana za mikopo kwa biashara Ndogo na za Kati.</li> <li>• Kuwepo kwa programu za kujenga uwezo kwa Biashara Ndogo na za Kati.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Biashara Ndogo na za Kati hazina dhamana za mikopo.</li> <li>• Ukosefu wa mali za biashara zilizorasimishwa zitakazoweza kutumika kama dhamana.</li> <li>• Matumizi ya chini ya huduma za fedha kwa kutumia teknolojia ya kidijitali.</li> <li>• Changamoto katika upatikanaji wa mikopo.</li> </ul>

Makundi ya Kipaumbele	Fursa	Changamoto
Watu wenye uhitaji maalumu	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Huduma za fedha za kidijitali hupunguza vikwazo vya upatikanaji kwa watu wenye ulemavu.</li> <li>• Mazingira wezeshi ya kisheria na udhibiti kwa watu wenye ulemavu</li> <li>• wepo wa vikundi na vyama vya watu wenye ulemavu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Njia za utoaji wa huduma za fedha zisizokidhi uhitaji kwa watu wenye ulemavu</li> <li>• Mbinu ya utoaji elimu ya fedha zisizokidhi uhitaji watu wenye ulemavu</li> <li>• Hatari kubwa inayodhaniwa na taasisi za fedha kuhusu kuwapatia huduma watu wenye uhitaji maalumu kama walemavu</li> <li>• Bidhaa chache za fedha zisizokidhi mahitaji ya watu wenye uhitaji maalum</li> <li>• Ushiriki wao mdogo katika shughuli za kiuchumi</li> </ul>

Makundi ya Kipaumbele	Fursa	Changamoto
Wakulima na Wavuvi wadogo wadogo	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuwepo kwa msaada kutoka Serikalini pamoja na washirika wa maendeleo ya kilimo</li> <li>• Kuwepo kwa mipango ya dhamana ya kilimo</li> <li>• Kuwepo kwa taasisi za ufadhili wa maendeleo ya kilimo</li> <li>• Kuwepo kwa vyama vya ushirika vya kilimo</li> <li>• Kuwepo kwa skimu za kilimo cha umwagiliaji</li> <li>• Uwepo wa rasilimali asilia za maji</li> <li>• Uwepo matumizi hafifu ya idadi kubwa ya samaki katika maji safi na ya baharini</li> <li>• Uwepo kwa fursa za utalii wa kiikolojia katika mazingira ya majini zikiwemo za maeneo ya ufugaji wa viumbe wa majini.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Miundombinu duni ya kilimo</li> <li>• Ukosefu wa mali zilizorasimishwa kutumika kama dhamana</li> <li>• Hatari kubwa ya upotevu wa maliasili kupitia shughuli za kilimo</li> <li>• Kiwango kidogo cha ufadhili wa kilimo</li> <li>• Upungufu wa fedha za kusaidia wavuvi wadogo</li> <li>• Mikakati duni ya uuzaji wa bidhaa za uvuvi</li> </ul>

# WADAU WA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA NA MUUNDO WA URATIBU

---

## Wadau wa Huduma Jumuishi za fedha

Utekelezaji wa Mpango Mkakati huu utahusisha wadau wengi wa Huduma Jumuishi za Fedha, mathalani Wizara na Mamlaka za kiserikali, taasisi za usimamizi katika Sekta ya fedha, taasisi za fedha, vyama na mitandao katika huduma za fedha, pamoja na wadau wa kimaendeleo katika nyanja ya huduma jumuishi za fedha. Kila mdau ana majukumu ya kipekee katika kuhakikisha Mpango Mkakati huu unatekelezwa.

## Muundo wa Uratibu

Mpango Mkakati huu unalenga kuwaleta pamoja wadau kutoka katika sekta ya umma na binafsi ili kushiriki kutimiza maono ya pamoja ya huduma jumuishi za fedha kupitia utaratibu ulioratibiwa. Mfumo wa muundo wa uratibu wa Mpango Mkakati huu upo katika ngazi tatu ambazo ni: Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za fedha, Kamati ya Taifa ya Uongozi wa Huduma Jumuishi za Fedha, pamoja na Kamati ya Taifa ya Kiutendaji ya Huduma Jumuishi za Fedha. Pamoja na kamati hizo, kuna Kamati ya Wanawake ya Huduma Jumuishi za Fedha ambayo ina kazi ya kulishauri Baraza la Taifa kuhusu masuala ya kukuza huduma jumuishi za fedha kwa wanawake nchini. Pia, Benki Kuu ni Sekretarieti ya Baraza la Taifa na Kamati zote zinazosimamia Huduma Jumuishi za fedha kitaifa.

## UFUATILIAJI NA TATHMINI

Utekelezaji wa malengo ya huduma jumuishi za fedha nchini unahitaji mfumo thabiti wa ufuatiliaji na tathmini ambao una rasilimali za kutosha na kukubalika na wadau wote. Mfumo wenye uwezo wa kuonyesha matokeo; kutambua vikwazo, pamoja na kuongoza ugawaji na matumizi ya rasilimali. Kwa sababu hiyo, Mpango Mkakati huu umeweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango inayolenga kuboresha matumizi ya huduma jumuishi za fedha na viashiria vya matokeo.

Uendeshaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utahakikisha kila taasisi husika inatekeleza mipango iliyokabidhiwa ndani ya muda uliowekwa kama ilivyoainishwa katika mpango wa utekelezaji, pamoja na kufuatilia viashiria husika kama ilivyoainishwa katika mfumo wa matokeo. Taasisi za utekelezaji wa Mpango Mkakati zitawasilisha matokeo ya utekelezaji kwa Sekretarieti kwa ajili ya uratibu kwa niaba ya Kamati

Tendaji ya Taifa ya Huduma Jumuishi za Fedha. Hivyo basi, utekelezaji wa Mpango Mkakati huu utahitaji uwekezaji katika kanzidata pamoja na tafiti zitakazowezesha upatikanaji wa taarifa kutoka wadau, taasisi, au jamii, zitakazosaidia kupima matokeo ya utekelezaji wa mipango ya huduma jumuishi za fedha ili kusaidia kamati zote kutoa maamuzi sahihi.

## **Mfumo wa Kupima Matokeo au Utekelezaji**

Mfumo wa kupima matokeo unaainisha viashiria muhimu na shabaha zitakazotumika kupima matokeo ya hatua zilizochukuliwa katika kufikia matokeo yanayotarajiwa kwenye masuala ya huduma jumuishi za fedha.

- Upatikanaji wa huduma za fedha utapimwa na kigezo cha ukaribu wa huduma katika jamii
- Utumiaji wa huduma za fedha utapimwa kwa uwepo wa bidhaa na huduma za kutosha na mzunguko au uwingi wa matumizi ya fedha,
- Ubora utapimwa kulingana na uwezo wa fedha kwa watumiaji, uwezo wa kumudu gharama na kufaa kwa bidhaa, pamoja na ufanisi wa kushughulikia malalamiko. Kwa upande mwingine,
- Ustawi wa fedha utapimwa kwa kuangalia uwezo wa watu binafsi na biashara katika kukidhi mahitaji ya sasa ya fedha, kudhibiti misukosuko ya fedha na kupanga mahitaji ya baadaye.

Vipimo vya matokeo au utekelezaji vimeambatishwa kwenye ukurasa ufuatao



# VIAMBATISHO

## Kipimio cha utekelezaji

KIPIMO	UFIKIAJI					
Lengo la kimkakati namba 1	Watu wote kufikiwa na watoa huduma za fedha					
Matokeo Mahususi namba 1.1	Watu wazima na biashara zote zinaweza kuhudumiwa na taasisi za fedha					
Kiashiria	Kipimo/Kiashiria	Msingi 2023	Lengo		Chanzo cha taarifa	Mzunguko wa ripoti
			Kati 2025	Mwisho 2028		
1.1.1	% ya watu wazima wanaoishi ndani ya kilomita 5 za pointi za huduma upatikanaji wa huduma za fedha.	89%	92%	95%	BOT/ Finscope	Miaka 2
1.1.2	% ya watu wazima walio na Utambulisho wa kipekee.	78%	63%	65%	NIDA	Kila Mwaka
1.1.3	% Biashara Ndogo na za Kati zilizo na usajili rasmi	10%	12%	15%	MITI	Kila Mwaka
1.1.4	% ya watu wazima wanaomiliki simu	71%	73%	75%	TCRA/NIDA	Kila Mwaka
1.1.5	% ya wakopaji wenye taarifa katika Mfumo rejea wa Mikopo.	30%	33%	35%	BOT	Kila Mwaka

1.1.6	% ya Biashara Ndogo na za Kati kama wakopaji walio na taarifa katika Mfumo Rejea wa Mikopo.	19%	22%	25%	BOT	Kila Mwaka
1.1.7	% ya watu wazima wanaotumia mtandao wa intaneti	31%	40%	50%	Finscope/TCRA	Miaka 3
Matokeo Mahususi namba 1.2	Watu wazima na wafanyabiashara wote wana akaunti katika taasisi za fedha					
1.2.1	% ya watu wazima walio na akaunti zinazoweza kufanya miamala katika taasisi za fedha	76%	80%	85%	Finscope	Miaka 3
1.2.2	% ya Biashara Ndogo na za Kati zilizo na akaunti katika taasisi za fedha	11%	13%	16%	Tafiti katika Biashara Ndogo na za Kati	Miaka 3

KIPIMO	MATUMIZI					
Lengo la kimkakati namba 2	Ongeza matumizi ya anuwai ya bidhaa na huduma za fedha					
Matokeo Mahususi namba 2.1	Wengi wa watu wazima na biashara kutumia bidhaa na huduma za fedha mara kwa mara					
2.1.1	% ya watu wazima wenye akaunti hai katika taasisi za fedha	60%	70%	75%	Finscope	Miaka 3
2.1.2	% ya Biashara Ndogo na za Kati zenye akaunti hai katika taasisi za fedha	11%	13%	16%	Tafiti katika Biashara Ndogo na za Kati	Miaka 3
Matokeo Mahususi namba 2.2	Wengi wa watu wazima na biashara hutumia anuwai ya bidhaa na huduma za fedha					
2.2.1	% ya watu wazima wanaotumia zaidi ya bidhaa moja ya fedha.	33%	45%	50%	Finscope	Miaka 3
2.2.2	% ya watu wazima waliowekeza katika masoko ya mitaji	2.4%	5%	10%	CMSA	Kila mwaka
2.2.3	% ya watu wazima wanaopata huduma za bima	10.3%	15%	20%	TIRA	Kila Mwaka
2.2.4	% ya watu wazima waliokopa katika taasisi za fedha	11%	20%	27%	Finscope	Kila mwaka
2.2.5	% ya Mikopo ya Biashara Ndogo na za Kati kwa uwiano wa Mikopo yote	12%	20%	25%	BOT	Kila mwaka
KIPIMO	UBORA					

Lengo la kimkakati namba 3	Kuboresha Ubora wa bidhaa na huduma za fedha					
Matokeo Mahususi namba 3.1	Watumiaji wa huduma za fedha wana imani na uaminifu kujihusisha na taasisi za fedha					
3.1.1	% ya watu wazima wanaojiamini kujihusisha na taasisi za fedha	56%	65%	70%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2
3.1.2	% ya watu wazima wenye ujuzi wa fedha	60%	65%	70%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2
3.1.3	% ya watu wazima wenye elimu fedha kwa njia za idigitali	40%	50%	55%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2
3.1.4	% ya taasisi za ndogo ndogo kukopesha zenye utaratibu wa kushughulikia malalamiko	5%	15%	30%	BOT	Kila mwaka
3.1.5	% ya malamiko yaliyoshughulikiwa na taasisi za fedha	85%	90%	95%	BOT	Kila Mwaka
Matokeo Mahususi namba 3.2	Huduma za fedha zina bei nafuu, zinapatikana kiurahisi na za kuaminika					
3.2.1	% ya watumiaji wa huduma za fedha wanaomudu gharama za kupata huduma	80%	85%	90%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2
3.2.2	% ya watumiaji wa huduma za fedha wanaoridhika na huduma za fedha zilizopo katika soko	80%	85%	90%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2

3.2.3	% ya watumiaji wa bidhaa na huduma za fedha wanye uwezo wa kuwasiliana na kusimamia haki zao toka kwa taasisi za fedha	75%	80%	85%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2
<b>KIPIMO</b>	<b>USTAWI</b>					
Lengo la kimkakati namba 4	Kuboresha ustawi wa fedha wa watu binafsi na biashara					
Matokeo Mahususi namba 4.1	Watu binafsi na biashara kukidhi mahitaji yao ya sasa					
4.1.1	% ya watu wazima wenye uwezo wa kulipa bili, madeni na majukumu mengine ya fedha kwa wakati	14%	20%	25%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2
4.1.2	% ya Biashara Ndogo na za Kati zenye uwezo wa kulipa bili, madeni na majukumu mengine ya fedha kwa wakati	3%	10%	15%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2
Matokeo Mahususi namba 4.2	Watu binafsi na biashara wanaweza kukabiliana na matukio yasiyotarajiwa					
4.2.1	% ya watu wazima wenye uwezo wa kupata pesa za dharura ndani ya siku 30 bila matatizo	55%	65%	70%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2

4.2.2	% ya Biashara Ndogo na za Kati zenye uwezo wa kupata pesa za dharura ndani ya siku 30 bila matatizo	71%	75%	80%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2
4.2.3	% ya Biashara Ndogo na za Kati zenye bima	4.4%	10%	15%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2
Matokeo Mahususi namba 4.3	Watu binafsi na biashara wanaweza kupanga kwa ajili ya siku zijazo					
4.3.1	% ya watu wazima waliowekeza katika rasilimali za fedha na halisi	28%	5%	40%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2
4.3.2	% ya watu wazima walio na akaunti za pensheni	3.6%	5%	10%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2
4.3.3	% ya Biashara Ndogo na za Kati mipango ya ufadhili wa dharura	50%	55%	60%	Tafiti za huduma jumuishi za fedha	Miaka 2





23

28

BARAZA LA TAIFA LA HUDUMA  
JUMUISHI ZA FEDHA